# MFUMO WA STAKABADHI ZA MAGHALA TANZANIA


## SHUKRANI

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni utaratibu ulioanzishwa kisheria wa kutumia mazao kwenye maghala kama dhamana ya kupata mikopo kutoka asasi za fedha. Mfumo huu ulianzishwa nchini Tanzania mnamo mwaka 2000 kwa kupitia utaratibu wa miradi na kufanyiwa majaribio katika maeneo mbali mbali nchini. Tunaupongeza Mfuko wa Mazao Duniani (Common Fund for Commodities- CFC) wenye makao yake makuu nchini Uholanzi kwa kuwezesha utekelezaji wa mfumo huu nchini.

Mfuko huu unashirikiana na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko na wadau katika sekta binafsi zikiwemo Asasi za fedha, Waendesha Maghala, Viwanda vya Kusindika mazao, Makampuni ya kusimamia dhamana pamoja na Bodi za mazao.

Tunapongeza uamuzi wa Serikali kuukubali mfumo huu utumike hapa nchini kwa kuwa mafanikio yaliyokwisha onekana ni dhahiri kuwa ni ukombozi mkubwa kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo na wakati. Pia tunapongeza uongozi wa Bodi ya leseni za maghala Tanzania Kwa kusimamia na kuendeleza utekelezaji wa mfumo huu hapa nchini.


## 1.0 UTANGULIZI


### 1.1 Tafsiri ya Mfumo

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni mfumo unaotumika nchini wa kutumia bidhaa zilizohifadhiwa kwenye maghala badala ya mali zisizohamishika kuwa dhamana ya kupata mikopo kutoka asasi za fedha. Mfumo kama huu pia unatekelezwa nchi nyingine za bara la Afrika pamoja na mabara ya Ulaya na Amerika.

Kwa kufuata mfumo huu wakulima wadogo na wakati wakiwa kwenye Ushirika au Vikundi vya wakulima wanakuwa na nguvu ya soko na kuingia katika soko la ushindani ambalo ingekuwa vigumu kutokana na kukosekana kwa mitaji. Pia mfumo huu unasaidia kuzuia upotevu wa mazao unaotokana na uhifadhi dhaifu, kuhifadhi mazao ili kusubiri kuuza wakati muafaka na pia kuongezea bidhaaa thamani kabla ya kuziuza.

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni mfumo unaotumika kisheria chini ya sheria No. 10 ya 2005 na kutekelezwa kwa kanuni za mfumo za 2006. Mfumo huu kwa sasa unatumika katika maeneo mbalimbali nchini kwa mazao ya kahawa, pamba, korosho, mahindi na mpunga/mchele.

## NAMNA MFUMO UNAVYOFANYA KAZI




### 1.2 LENGO LA KUANZISHWA MFUMO HUU NCHINI TANZANIA:

- Kuongeza mafao kwa mkulima mdogo na wakati kwa kuongeza uwazi na ufanisi wa mfumo wa masoko ndani ya soko huru
- Kuimarisha biashara na soko la mazao kwa kuongeza ufanisi katika ubora wa mazao na kuimarisha mfumo wa ukusanyaji uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu
- Kuwapa wakulima nguvu ya soko kwa kuhamasisha utumiaji wa Ushirika au Vikundi vya wakulima.
- Kutoa mafunzo ya kibiashara kwa wadau mbalimbali watakaoutumia mfumo huu
- Kuwezesha utumiaji wa mazao kwenye maghala kama dhamana ya kupata mikopo kutoka Asasi za fedha

## 2.0 WADAU WAKUU NA MAJUKUMU YAO KATIKA MFUMO

Mdau ni mtu au kikundi chenye wajibu kuhusiana na uendeshaji wa mfumo wa stakabadhi za maghala ambao ni:

### 2.1 Mweka Mali

Mweka mali ghalani anaweza kuwa ni Mtu binafsi, Kampuni binafsi, Kikundi cha wakulima au Chama cha Ushirika. Majukumu yake ni pamoja na:

- Kujua ghala atakalohifadhi mazao yake
- Kukusanya bidhaa, kuziwekea bima dhidi ya moto, wizi na hatari mbalimbali na kuzisafirisha hadi kwenye ghala lililokubalika kisheria kwa ajili ya kuhifadhi bidhaa hizo kwa malengo mbali mbali.

- Kupewa Stakabadhi mara afikishapo bidhaa kwenye ghala ikionyesha wingi na ubora wa bidhaa hiyo. Stakabadhi za Maghala ni utambulisho wenye thamani ya kifedha ya kuonyesha wingi na ubora wa bidhaa zilizohifadhiwa katika ghala ambazo hutumika pia kupata mkopo kutoka asasi za fedha.
- Kulipa kwa Mwendesha ghala gharama za kuhifadhi na gharama nyingine zitakazoambatana na uhifadhi wa bidhaa hiyo kwenye ghala.
- Kuondoa bidhaa zake kwenye ghala kwa ajili ya kuuzwa au kwa shughuli nyingine baada ya Mwendesha ghala kupata vielelezo vya kuridhisha kutoka kwa Mweka mali na kwa Asasi iliyotoa mkopo.

**2.2 Mwendesha Ghala**

Mwendesha ghala anaweza kuwa ni mwenye ghala au aliyekodisha kwa mwenye ghala. Inaweza kuwa ni Kampuni, Chama Kikuu cha Ushirika au cha Msingi ambacho kina nia na uwezo wa kufanya kazi ya uendeshaji wa ghala. Mwendesha ghala anapaswa kuomba leseni ya uendeshaji wa ghala kwa Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania.

Mwombaji wa kuendesha ghala anapaswa awe na vithibitisho vifuatavyo: umiliki au ukodishaji wa ghala, Katiba na kanuni za kampuni, Mpango wa makadirio ya biashara, Hati ya kuandikishwa kufanya biashara, Barua ya utambulisho kutoka benki yeyote inayoonesha kuwa ni mteja, Leseni ya biashara, Picha mbili za viongozi ikiwemo za Mkurugenzi na mtumishi mmoja wa kampuni zilizothibitishwa na mwanasheria, pamoja na taarifa zingine zozote muhimu kuthibitisha kuwepo kwa biashara. Majukumu ya mwendesha ghala ni pamoja na:

- Kupokea bidhaa zilizoletwa kwenye ghala, kuzipima uzito, kuhakikisha ujazo ubora kabla ya kuingiza ghalani
- Kutoa Stakabadhi yenye taarifa zote muhimu kwa Mweka mali mara afikishapo bidhaaa kwenye ghala
- Kuhakikisha kuwa ghala linalotumika pamoja na mazao yaliyohifadhiwa yamewekewa bima dhidi ya moto na hatari nyinginezo
- Kuhakikisha usafi wa ghala kwa kufukiza dawa kabla ya kuhifadhi bidhaa
- Kuhakikisha mazao yanayoingizwa ghalani yamefukizwa dawa kwa taratibu na kanuni za viwango vinavyokubalika wa hifadhi ya chakula
- Kuhakikisha kuwa taratibu za kuhifadhi bidhaa zinafuatwa na upangaji wa mizigo ghalani zikionesha utambulisho utakaomuwezesha mkaguzi kufanya kazi yake kwa urahisi
- Kutoa taarifa sahihi kwa asasi za fedha zinazotoa mikopo kuhusu bidhaa zilizohifadhiwa
- Kusaini mkataba wa utendaji (performance bond) na Bodi ya Leseni za Maghala kabla ya kuweka mazao kwenye ghala
- Kupeleka taarifa zinazohitajika Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania
- Kuhakikisha kuwa bidhaa zilizohifadhiwa zinabaki katika ubora kama wakati zilipoingia au kuwa na ubora zaidi.
- Kuhakikisha kuwa anao wataalamu wenye ujuzi wa kuhifadhi bidhaa
- Kuruhusu bidhaa iondolewe kwenye ghala baada ya kupata vielelezo inavyotakiwa

- Kutunza taarifa na Vitabu vya Stakabadhi katika sehemu ya usalama (Kasiki)
- Kuhakikisha ghala lina vifaa muhimu vikiwemo vifaa vya kuzima moto, chaga, mizani iliyokaguliwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo, na vitabu muhimu vya kupokelea na kutoa mizigo

**2.3 Asasi za Fedha**

Asasi za fedha zinaweza kuwa ni Benki za Biashara, Benki za Jumuiya, benki za kuweka na kukopa za ushirika (SACCOS/SACAS) Benki Kata au Kampuni na Asasi zisizo za serikali zilizosajiliwa kwa mujibu wa sheria. Kazi za taasisi za fedha ni pamoja na:

- Kuwa na taarifa za kutosha kuhusu Mweka mali, Mwendesha ghala na bidhaa zitakazohifadhiwa
- Kutoa mkopo kwa Mweka mali mara anapopelekewa stakabadhi ya Dhamana
- Kutoa maelekezo kwa Mwendesha ghala ya kuruhusu utoaji wa bidhaa kwenye ghala
- Kutoa mkopo unaozingatia bei na gharama zote atakazotumia Mweka mali hadi kufikisha bidhaa kwenye ghala
- Kutoa elimu kwa wateja wake (Mweka mali) hasa kuhusu masharti ya mikopo na jinsi ya kujikinga na mabadiliko ya bei

**2.4 Serikali**

**2.4.1 Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania**

Bodi ya kusimamia mfumo itakuwa ni chombo kilichoundwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazohusu matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala zinatekelezwa ipasavyo kulingana na sheria ya mfumo No. 10 ya 2005 na Kanuni zake za mwaka 2006.

**Dira ya Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania ni** Kuwa taasisi inayowaunganisha wakulima na mifumo rasmi ya mikopo na masoko kwa kutumia mfumo madhubuti na wenye ufanisi wa Stakabadhi za Maghala

**Dhima ya Bodi**:

Kudhibiti na kuendeleza Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ambao utahakikisha ushindani wa haki na endelevu kwa kutumia mifumo rasmi ya mikopo na masoko. Aidha majukumu ya bodi ya leseni Tanzania ni pamoja na:

- Kusimamia mfumo wa Stakabadhi za Maghala.
- Kutoa leseni kwa wenye maghala, waendesha Maghala na Wakaguzi wa maghala
- Kuhakiki Stakabadhi za maghala zitakazotumika na kuhakikisha zimetayarishwa kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa
- Kuwa na wataalamu wenye ujuzi katika shughuli za masoko kwa ujumla na katika kuhifadhi bidhaa kwenye maghala
- Kuhakiki mkataba wa mwendesha ghala ili kujiridhisha kuwepo kwa makubaliano ya kiutendaji (performance bond)
- Kupata ruzuku kutoka Serikali kuu na kutafuta vyanzo vingine vya mapato
- Kutoa elimu ya mfumo kwa wadau mbalimbali

**Utoaji Elimu kwa wakulima kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa njia ya mazungumzo na kutumia vijarida,**



**Wakulima wa Malula Meru wakipatiwa ufafanuzi kuhusu uendeshaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala**

### 2.4.2 Halmashauri za Wilaya

- Kutoa ushauri kwa wakulima kwa kutumia wataalamu walio chini yake kuzalisha bidhaa zilizo bora
- Kuweka utaratibu wa ukusanyaji ushuru utakaoendana na matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala
- Kuweka katika bajeti zake utaratibu wa kuimariasha miundombinu (barabara, maghala/ magulio)
- Kusaidiana na Bodi kutoa elimu ya mfumo kwa wananchi

## 3.0 MAENEO YANAYOTUMIA MFUMO HUU NCHINI KWA SASA

Maeneo yanayotumia Mfumo huu ni pamoja na mikoa inayolima kahawa ya Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma na Kigoma; Mikoa ya Manyara na Shinyanga kwa zao la pamba; Mikoa ya Morogoro, Manyara na Kilimanjaro kwa zao la mpunga na Mkoa wa Mtwara , Pwani na Lindi kwa zao la korosho.Aidha, Benki za CRDB, NMB, Kilimanjaro Cooperative Bank (KCB), Uchumi Commercial Bank na Federal Bank of Middle East (FBME) wameshiriki kutoa mikopo chini ya mfumo huu.

### 3.1 Zao la Kahawa:

Wakulima katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma na Kigoma wametekeleza mfumo huu tangu msimu wa 2002/2003. Maghala ya TCCCO, MBICCO, MBOCCO na Kanyovu Joint Venture-Kigoma yanatumika katika Mfumo huu katika msimu wa

2008/09. Jumla ya maghala matatu mapya yameomba kusajiliwa kwa ajili ya kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Maghala hayo ni City Coffee –Mbeya, DAE Ltd-Mbinga na Mbinga Coffee Curing Co.Ltd –Makambako



**Ghala la TCCCO Kilimanjaro ni miongoni mwa maghala makubwa yanayotumika kutunza zaidi ya zao moja chini ya Mfumo huu.**

### 3.2 Zao la Pamba:

Chama cha Ushirika cha Msingi cha Oridoy kilichoko wilaya ya Babati, mkoa wa Manyara wanafaidika na mfumo huu. Ghala na jineri ya KNCU-Moshi limetumika kuhifadhi na kuchambua pamba mbegu. Aidha vyama vya Ushirika vya Msingi mkoani Shinyanga vimeanza kutumia Mfumo huu kuanzia msimu wa 2007/08 kwa kuhifadhi na kuchambua pamba katika jineri ya Uzogore chini ya mwendesha ghala –SIBUKA FM LTD.




Jengo la Chama cha Msingi Oridoy-Babati lililojengwa kutokana na mafanikio ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala

### 3.3. Zao la Mpunga

Wakulima wilayani Kilombero chini ya vikundi vya wakulima/Vyama vya Ushirika vya Msingi (29) wamenufaika katika mfumo huu kwa kuhifadhi mpunga katika ghala chini ya mwendesha ghala 'Kilombero High Quality Rice'. Aidha, msimu wa 2007/08 wakulima wa mpunga wilaya ya Moshi kupitia chama chao cha CHAWAMPU wameanza kuhifadhi mchele katika ghala la TCCCO – Moshi kwa kutumia Mwendesha ghala ambaye pia anahifadhi kahawa.

Uendeshaji wa mfumo huu pia umeigwa na kuendeshwa na program mbalimbali ikiwemo ya MRSP kupitia mpango wa benki mazao yakiwemo maeneo ya Magugu-Babati, Masakta-Hanang, Mbarali n.k. Juhudi hizi zinahitaji kuimarishwa ili kukidhi vigezo vya uendeshaji wa mfumo kwa mujibu wa mwongozo wa uendeshaji uliotolewa na Bodi ya Leseni za Maghala Tanzania.



**Uhifadhi wa mazao ghalani unaoendeshwa na SACCOs ya Mshikamano Magugu-Babati**

### 3.4. Zao la Korosho

Msimu wa 2007/08, Mfumo wa Stakabadhi za Maghala umeanza kutekelezwa katika zao la korosho Mkoani Mtwara. Jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi 164 vimewezeshwa kutumia mfumo huu, Aidha msimu wa 2008/2009 Mfumo umetekelezwa pia mkoani Mtwara na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Lindi na Pwani. Wakulima wa mkoa wa Lindi wamefaidika na mfumo huu, kwa mfano Chama cha Ushirika cha Umoja Liwale wamefanikiwa kununua trekta la chama na kiasi cha fedha kutumika katika maandalizi ya ujenzi wa ghala. Chama cha Ushirika cha Msingi Luchelegwa wilayani Rungwa pia kimeweza kuuza korosho na kununua lori kwa ajili ya usafirishaji.

## 4.0 NGUZO MUHIMU ZA UTEKELEZAJI WA MFUMO

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala una nguzo kuu zifuatazo**:-**

**4.1. Upatikanaji na usambazaji wa taarifa**. Taarifa za bidhaa zilikohifadhiwa, ubora wake na bei pamoja na wanunuzi wa bidhaa ni mojawapo ya taarifa muhimu zitakazohitajika. Taarifa ya sehemu yaliko maghala na waendesha maghala. Asasi za Fedha zinazotoa mikopo zitahitaji kupata taarifa za mara kwa mara juu ya bidhaa zilizohifadhiwa kwenye ghala.

**4.2. Uimarishaji wa ubora wa bidhaa.** Bidhaa zitakazokuwa zinapokelewa kwa ajili ya kuhifadhiwa zitatakiwa kuwa na ubora kwa kufuata viwango vitakavyokuwa vimewekwa na Bodi ya kusimamia mfumo**.** Mwendesha ghala atahakikisha kuwa bidhaa zilizohifadhiwa kwenye ghala zinabaki na ubora kama zilivyoletwa au kuzidi. Pia bidhaa zinazohifadhiwa kwenye maghala zinaongezewa ubora kwa kuzisindika.

**4.3. Maghala yenye ubora.** Mfumo wa Stakabadhi za Maghala unatumia maghala yaliyokaguliwa na kupewa leseni. Leseni zitatolewa tu kwa maghala yaliyo na ubora na ambayo yana vifaa muhimu kama itakavyoshauri Bodi na wakaguzi wa maghala.




**Maghala ya vijijini yakiimarishwa yatawezesha utekelezaji wa mfumo kama mradi wa WIC unavyotarajia kufanya ukarabati wa ghala hili la Gendi –Babati ili kuanza utekelezaji wa mfumo.**

**4.4. Usimamizi wa Sheria na Kanuni za mfumo.** Mfumo wa Stakabadhi za Maghala umeanzishwa kisheria na unasimamiwa na Sheria No 10 ya 2005. Majukumu ya kila mhusika kwenye mfumo yameainishwa na adhabu zitakazotolewa kwa kukiuka Sheria nazo zimetolewa na zitasimamiwa na Bodi. Kanuni za sheria hiyo pamoja na Kitabu cha Mwongozo (Operational Manual) cha uendeshaji wa shughuli za mfumo vitatumika pia katika utekelezaji wa mfumo huu.

**4.5. Upatikanaji wa masoko ya kuuzia bidhaa.** Mweka mali ana jukumu la kujua ni wapi atakapopata soko wakati anapokuwa amehifadhi bidhaa kwenye ghala. Bodi,

Mwendesha Ghala Asasi za fedha n.k zinaweza pia kusaidia kutafuta masoko ya bidhaa zilizohifadhiwa iwapo Mweka mali atahitaji msaada huo.

**4.6. Bima ya bei.** Mfumko wa bei kwa mazao yanayolimwa hapa nchini na hasa katika soko la dunia ni jambo ambalo linaathiri sana bei. Ili kuondokana na tatizo hili na hasa chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, ni vyema mweka mali akajiwekea utaratibu wa kukinga bei hata kabla ya kukusanya mazao na kuyapeleka kwenye ghala. Kwa kufanya hivyo itamsaidia mweka mali kujua kiasi ambacho atapata baada ya kuuza mazao hayo. Kinga ya bei inaweza kuwa kwa njia ya kutumia bima ya bei katika mpango wa soko la baadaye.

## 5.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MFUMO

### 5.1. Elimu kwa wadau

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala ni mfumo unaowahusisha wadau mbalimbali wakiwemo Waendesha maghala, Asasi za fedha, Waweka mali na Serikali. Kwa kuwa mfumo huu ni mpya, uelewa wa jinsi unavyofanya kazi bado hautoshelezi.

### 5.2. Miundombinu ya kuuwezesha mfumo ufanye kazi

Miundombinu katika mfumo huu haitoshelezi kiasi cha kuwezesha mfumo huu ufanye kazi kwa ufanisi. Barabara kutoka sehemu za uzalishaji hadi kwenye maghala ya kuhifadhia bidhaa, nyingi hazipitiki wakati wa mvua, maghala yaliyo mengi karibu na wakulima hayajafikia kiwango kinachotakiwa kupata leseni ya kuhifadhi bidhaa na mengine yenye ubora hayatumiki ipasavyo.

### 5.3. Udhaifu wa Mfumo wa Ukusanyaji, Usambazaji wa taarifa na Takwimu chini ya mfumo.

Mawasiliano kwa ajili ya upashanaji habari hayatoshelezi**.** Upatikanaji taarifa ni kiungo cha kuwaunganisha wadau watakaotumia mfumo wakiwemo waweka mali, Waendesha maghala, Bodi, Asasi za fedha na hata Wanunuzi.

### 5.4. Ufinyu wa viwanda/vinu vya kusindika mazao

Kukosekana kwa viwanda vya kusindika mazao kunaathiri uuzaji wa bidhaa zetu kwa bei nzuri. Mazao yanaposindikwa yanaongezeka thamani na pia soko. Chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, ni mazao yenye ubora wa kutosha ndiyo yatakubalika kuhifadhiwa. Usindikaji wa mazao unatiliwa mkazo chini ya mfumo huu.

### 5.5. Wakulima wengi kutokuwa na imani na ushirika.

Wakulima walio wengi wa mazao ya kilimo hapa nchini ni wadogowadogo ambao kiasi wanachovuna ni kidogo. Ili mfumo huu uwe wa manufaa unahitaji upunguze gharama za uendeshaji. Kwa wakulima wadogo ili waweze kupunguza gharama inawabidi kujiunga kwenye Vikundi au Vyama vya Ushirika ili kiasi watakachokusanya kiwe kingi kuweza kupunguza gharama kama za usafirishaji, uhifadhi na usindikaji.

### 5.6. Kukosekana kwa viwango kwa mazao yetu.

Mazao yaliyo mengi hapa nchini yanauzwa bila kutumia viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Aidha viwango kwa mazao mengine havipo au kama vipo havitumiki ipasavyo. Kwa kutumia mfumo huu inahitaji kutumia viwango vilivyopo ambavyo vinakubalika katika masoko ya ndani na ya nje ya nchi.

**5.7. Usimamizi wa matumizi ya Sheria ya mfumo**

Katika kutekeleza Mfumo wa Stakabadhi za Maghala Sheria iliyowekwa kwa ajili ya kusimamia mfumo inaweza kutumika visivyo au kugongana na Sheria nyingine zilizopo. Elimu ya kuwezesha watumiaji wa mfumo huu kufuata Sheria bado haijatosheleza.

**5.8. Kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kuuza bidhaa zilizohifadhiwa kwenye maghala**

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala utakuwa endelevu na wenye ufanisi endapo utaanzisha Soko la pamoja la kubadilishana Stakabadhi kama njia ya kuuza bidhaa. Mnunuzi atanunua bidhaa kwa kupewa stakabadhi bila ya kuona bidhaa zilizohifadhiwa kwenye ghala na patakuwepo na ushindani ili kutoa fursa kwa Waweka mali kupata bei nzuri.

**5.9. Uwezo wa Waendesha maghala**

Uwezo wa Waendesha maghala unaambatana na kuwepo kwa udhibiti wa viwango (performance guarantee/insurance bond) ambayo ni njia ya kufidia bidhaa zitakazoharibika kutokana na uzembe utakaosababishwa na Mwendesha ghala.

**5.10. Imani ya Mabenki katika mfumo mzima**

Mfumo wa Stakabadhi za Maghala unahimiza kuwepo kwa benki nyingi zitakazoleta ushindani na hivyo unafuu kwa wale watakaoomba mikopo. Hadi sasa ni benki chache zinashiriki katika mfumo huu kwa kuwa nyingi bado hazina imani na kukopesha wakulima/wafanya baishara wadogo**.**

**6.0 UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZILIZOTAJWA:**

6.1 Bodi ya leseni za Maghala kutayarisha programu ya kutoa elimu na kufanya uhamasishaji. Aidha, Bodi kushirikiana na taasisi za elimu kuanzisha mitaala ya kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu mfumo. Mfano, kushirikisha vyuo vya SUA-Morogoro, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu Dodoma, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru na MUCCOBS-Moshi nk.

6.2 Sekta binafsi kuhamasishwa kuwekeza katika ujenzi wa maghala ambayo yatatumika kuimarisha mfumo.

6.3 Kubuni mbinu za uuzaji wa bidhaa zilizohifadhiwa kwenye maghala kama kuwepo kwa soko la pamoja (Agricultural Commodity Exchange )

6.4 Serikali kuhamasisha usindikaji wa bidhaa zitakazohifadhiwa kwenye maghala ili kuongeza wigo wa soko na kupata bei nzuri.

6.5 Bodi kuwa na mipango ya baadaye ya kuanzisha matawi kwenye kanda kulingana na kuongezeka kwa matumizi ya mfumo ili kurahisisha utoaji huduma kwa walengwa.

6.6 Bodi kushirikiana na taasisi zinazohusika na uwekaji wa viwango kwa bidhaa zitakazohifadhiwa kwenye maghala

6.7 Bodi kutoa adhabu kali kwa wale watakaokiuka Sheria hii. Aidha Bodi isimamie uoanishaji wa Sheria ya mfumo na Sheria nyingine zinazohusiana na mfumo huu (mfano Sheria za Bodi ya mazao) ili kuondoa migongano.

6.8 Serikali kuu na Halmashauri za wilaya kuimarisha miundombinu kama barabara na maghala ili kuwezesha mfumo kufanya kazi vizuri

6.9 Halmashauri za wilaya kuhamasisha wakulima wajiunge kwenye vikundi vya uzalishaji mali na ushirika mbalimbali ili waweze kuingia kwenye mfumo wa stakabadhi za maghala kwa urahisi



**Ghala la kijiji cha Masakta –Wilaya ya Hanang lililoboreshwa kwa uendeshaji wa Mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani**

## 7.0. MATARAJIO YA BAADAYE

7.1. Bodi ya Leseni Tanzania kuwezesha Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kutumika katika mazao mengi ya kilimo na mazao mengine yasiyo ya kilimo

7.2. Mazao mengi yanayozalishwa kusindikwa kabla ya kuuzwa

7.1 Upotevu wa mazao unaotokana na uhifadhi hafifu kupungua au kwisha kabisa.

7.2 Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kuwa kichocheo katika kuchangia kupunguza umaskini na kuongeza uchumi wa nchi kutokana na wakulima kuongeza uzalishaji.

7.3 Ongezeko la ajira hasa kwa vijana kutokana na kuwepo kwa mahitaji ya wafanyakazi katika maghala na viwanda vya kusindika mazao.

7.4 Ongezeko la ajira vijijini kwa vijana kujiajiri katika kilimo kutokana na wakulima kupata bei itakayowapatia faida

7.5 Wakulima watakuwa na Umoja hivyo kuwa na sauti moja na kutetea haki zao

7.6 Kuwa na data base ya mazao yanayozalishwa na kuuzwa kwenye soko katika ngazi za jamii, wilaya, mkoa na taifa

7.7 Mfumo wa Stakabadhi kutumika pia katika upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima.

..……………………………………………………………………………

Imetolewa http://www.wrs.go.tz/downloads/newsletter/mfumo.pdf

08/10/2018